

HABARI KITAIFA

Waziri aeleza umuhimu sekta binafsi mifugo

Na Mbaraka Kambona

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema sekta ya binafsi ndiyo msingi wa maendeleo ya mifugo kwa sababu ushiriki wake umekuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza sekta hiyo nchini.

Waziri Ndaki alitoa kauli hiiyo jazi alipotembelea kiwanda cha kuchakata maziwa cha ASAS Dairies kilichoko mkoani Iringa.

Akiwa khandani hapo, alisema wawekezaji katika sekta

ya mifugo kama ASAS wakiwa wengi, ni jambo zuri kwa maendeleo ya uchumi wa nchi kwa sababu uzalishaji wanaoufanya unachangia ukuaji wa pato la taifa na kujenga afya za wananchi.

"Serikali tunajivunia kuwa na wazalishaji wa maziwa kama ninyi. Serikali tunawaahidi tuko pamoja nanyi ili kuinua uchumi wa nchi yetu," alisema Ndaki.

Aliongeza kuwa serikali iko macho kuangalia changamoto zinazowakabili wawekezaji na kuhakikisha zinapungua

makali yake ili kufanya kazi kwenye mazingira mazuri pamoja na wadau wao.

Kuhusu unywaji mdogo wa maziwa nchini, Waziri Ndaki alisema serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, imeshianza kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhamasisha unywaji wa maziwa ili wananchi wajenge utamaduni wa kunywa maziwa kwa wingi. Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha ASAS, Fuad Jaffer, alipongeza serikali kwa kuweka togo kwa bidhaa zinazotoka nje jambo am-

balo llimewapa wawekezaji wa ndani moyo wa kuendelea kuwekeza zaidi katika sekta ya mifugo.

Pia aliomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushirikisha vyuo vinavyozalisha maafisa ugani na taasisi za utafiti kuwa wabla na wachakataji wa maziwa ili kuzielewa changamoto ambazo wanazipata wafugaji.

Alisema kwa kufanya hivyo, wataalamu hao wanaweza kuwa msaada mkubwa katika kuelimisha wafugaji kuzalisha maziwa yenye ubora.



Livestock and Fisheries minister Mashimba Ndaki (2nd-L) pictured yesterday being taken around Iringa-based ASAS Dairies Ltd, a private dairy processing firm established in 2000 to provide high-quality milk products to the Tanzanian market. Photo: Correspondent Mbaraka Kambona

The Guardian Jan 7, 2022

Sekta binafsi yasifiwa maendeleo ya mifugo

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

MWANANCHI Jan 7, 2022
Iringa. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema sekta binafsi ndiyo msingi wa maendeleo ya mifugo nchini.

Waziri Ndaki alitoa kauli hiyo alipotembelea kiwanda cha kuchakata maziwa cha Asas mkoani hapa juzi.

Alisema wawekezaji kwenye sekta ya mifugo wakiwa wengi, ni jambo zuri kwa maendeleo ya uchumi kwa kuwa wanachangia ukuaji wa pato la Taifa.

"Serikali tunajivunia kuwa na wazalishaji wa maziwa kama ninyi, tunawaahidi tuko pamoja nanyi ili kuinua uchumi wa nchi yetu," alisema Ndaki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Asas, Fuad Jaffer aliipongeza Serikali kwa kuweka tozo za bidhaa zinazotoka nje, jambo linalowapa wawekezaji wa ndani moyo wa kundelea kuwekeza katika sekta ya mifugo.

Aliiomba Serikali kushirikisha vyyo vinavyozalisha maofisa ugani na taasisi za utafiti kuwa wabia na wachakataji maziwa ili kuzielewa changamoto wanazozipata kwa wafugaji.

Waziri aeleeza umuhimu sekta binafsi mifugo

Na Mbaraka Kambona

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema sekta ya binafsi ndiyo msingi wa maendeleo ya mifugo kwa sababu ushiriki wake umekuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza sekta hiyo nchini.

Waziri Ndaki alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea kiwanda cha kuchakata maziwa cha ASAS Dairies kilichoko mkoani Iringa.

Akiwa kiwandani hapo, alisema wawekezaji katika sekta

ya mifugo kama ASAS wakiwa wengi, ni jambo zuri kwa maendeleo ya uchumi wa nchi kwa sababu uzalishaji wanaoufanya unachangia ukuaji wa pato la taifa na kujenga afya za wananchi.

"Serikali tunajivunia kuwa na wazalishaji wa maziwa kama ninyi. Serikali tunawaahidi tuko pamoja nanyi ili kuinua uchumi wa nchi yetu," alisema Ndaki.

Aliongeza kuwa serikali iko macho kuangalia changamoto zinazowakabili wawekezaji na kuhakikisha zinapungua

makali yake ili kufanya kazi kwenye mazingira mazuri pamoja na wadau wao.

Kuhusu unywaji mdogo wa maziwa nchini, Waziri Ndaki alisema serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, imeshaanza kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhamasisha unywaji wa maziwa ili wananchi wajenge utamaduni wa kunywa maziwa kwa wingi. Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha ASAS, Fuad Jaffer, aliipongeza serikali kwa kuweka tozo kwa bidhaa zinazotoka nje jambo am-

balo limewapa wawekezaji wa ndani moyo wa kuendelea kuwekeza zaidi katika sekta ya mifugo.

Pia aliiomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushirikisha vyuo vinavyozalisha maofisa ugani na taasisi za utafiti kuwa wabia na wachakataji wa maziwa ili kuzielewa changamoto ambazo wanazipata wafugaji.

Alisema kwa kufanya hivyo, wataalamu hao wanaweza kuwa msaada mkubwa katika kuelimisha wafugaji kuzalisha maziwa yenye ubora.

By Guardian Reporter

LIVESTOCK and Fisheries Minister, Mashimba Ndaki has said the private sector is the foundation for development in the livestock sector because its involvement has been a great contribution in its development in the country.

Ndaki made the remarks on Wednesday this week during his inspection visit of ASAS Dairies Limited, the Iringa based milk processing plant.

He said it would be a good thing for the country's economic development if we have many investors in the livestock sector like ASAS Dairies because their production contributes to the growth of the national income and improving people's health. "The government is proud to have milk processors like you and we, as government assure you that we will work together in pursuing national economic growth.

He added that the government understands challenges facing investors and was working on them to reduce their severity.

In regard to small level of milk drinking in the country, Ndaki said the government, in collaboration with the private sector has embarked in the implementation of various strategies to mobilise milk drinking

Private sector a sure foundation for livestock sector development - Ndaki

among Tanzanians.

For his part, ASAS Dairies Managing Director, Fuad Jaffer hailed the government led by President Samia Suluhu Hassan for imposing import duties on milk products, the decision that has given local investors the urge to continue investing in the livestock sector.

He also appealed to the government, through the Livestock and Fisheries Ministry to incorporate colleges producing agricultural extension officers, as well as other research institutes to be partners in milk processing ventures in the country in order to understand the challenges facing livestock keepers.

*THE GREAT IAD
Jan 7, 2022*



EXPRESSION OF INTEREST (EOI) FOR MEDICAL INSURANCE COVER.

VSO CONTRACT OPPORTUNITY

VSO is a global voluntary organisation whose mission has been to bring people together to fight poverty through the lasting power of volunteering.

We will be running a tender process with the intention of awarding a contract for the provision of Medical Insurance Cover for VSO staff and their dependents and we are seeking expressions of interest from suitably experienced health insurance companies licensed by the Tanzania Insurance Regulatory Authority and eligible to provide medical insurance cover services in Tanzania.

VSO's requirements:

- Suppliers must be registered by Tanzania Insurance Regulatory Authority.

All expressions of interest must be received by VSO by **January 27, 2022, at 10:00hrs** and must be submitted electronically to the following email address: Tender.Tanzania@vsoint.org. The EOI must include a contact name, company name, company address, phone, and email address.

Tender documents will be sent to those who expressed an interest, following the close of the EOI period.

Anticipated contract/ agreement start date: April 1, 2022

Meneja Mwandamizi wa wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Ali Ngingite akizungumza wakati wa kucheza drao ya kwanza ya kampeni ya MastaBata Kivyakovyako iliyochezeshwa Dar es Salaam. Kutoka kushoto ni Meneja Mwandamizi Kitengo cha Kadi, Manfred Kayala, Msimamizi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Joram Mtafya na kulia ni Doleen Msonda wa Idara ya Kadi wa Benki ya NMB (Na Mpiga Picha Wetu).

Wafugaji washauriwa kufuga kibiashara

RAJA MUEBA
Jan 7, 2022

Na Mbaraka Kambona, Iringa

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewashauri Wafugaji nchini kufuga kibiashara na kuachana na ufugaji wa kuchunga ambao tija yake imekuwa ndogo kwao wenyewe na hata kwa Taifa pia.

Waziri Ndaki alitoa rai hiyo jana alipotembelea Shamba la kisasa la mifugo la Shaffer lililopo mkoani Iringa.

Akiwa katika shamba hilo akikagua shughuli mbalimbali zinazoendelea kwenye eneo hilo, alisema kuwa wanawashauri wafugaji kuanza kufuga kisasa na kuachana na ufugaji wa kiasili ambao sasa umeanza kupitwa na wakati.

"Tumekuwa hatuoni faida kwa mifugo yetu kwa sababu ya kung'a ng'ania ufugaji wa kiasili, wafugaji tuanze kufuga kibiashara ili tuongeze tija ya mifugo yetu," alisema Ndaki

Aliongeza kuwa ili waanze kuona tija ya ufugaji wao, lazima wabadilike na waache ufugaji wa kuzunguka kutafuta maeneo ya malisho na badala yake wawe na maeneo yao ya kufugia ambayo yatakuwa rahisi kufikiwa na Wataalamu kwa ajili ya

kuwapatia huduma zinazohitajika kwa mifugo yao.

Naye, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Bashiru Muhoja alisema kuwa Mwekezaji wa shamba hilo la mifugo la Shaffer anauhitaji mkubwa wa chakula cha mifugo yake kama vile soya na mahindi.

"Mhe. Waziri huyu mfugaji anauhitaji mkubwa wa soya, mahindi na alfaalfa ambapo kwa sasa vyote anavitoa nchini Zambia, hii ni fursa kwa wananchi wetu na tumeshaanza kuchukua jitihada na tunaorodha ya wakulima ambao wapo tayari kulima mazao hayo kwa ajili ya kumuuzia mfugaji huyu", alisema Muhoja

Kwa upande wake, Msimamizi wa Shamba la Shaffer, Mahboob Malick alisema kuwa wanaishukuru Serikali kwa ujumla kwa ushirikiano mkubwa inaowapatia na kwamba wako tayari kuendelea kushirikiana nayo kwa lengo la kuboresha ufugaji hapa nchini.

"Mhe. sisi tuko tayari kupokea vijana ambao wanataka kujifunza ufugaji waje hapa tutawafundisha namna bora ya ufugaji wa kisasa ili wakipata ujuzi huu waende kuwafundisha na wenzao na hatimaye kuboresha ufugaji wetu", alisema Malick.